OFISI YA RAISI – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA
SHULE YA SEKONDARI IHONGOLE

S.L.P. 411,
MAFINGA.
18/12/2020.

KUMB.Na.IHSS/MAF/F.I/2021/VOL.6

JINA LA MWANAFUNZI

_____

_____

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IHONGOLE MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

- Napenda kutumia nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA KWANZA** katika Shule hii mwaka **2021**.
- Shule hii iko katika mji wa Mafinga katika Mtaa wa Ihongole karibu na Kituo cha Afya Ihongole,barabara ya mkato kuelekea Kijiji cha Ndolezi.
- Shule hii ipo katika Kata ya Boma,Halmashauri ya Mji Mafinga.
- Shule ni ya Kutwa,yenye mchanganyiko Wavulana na Wasichana.
- Hali ya hewa na Mazingira ni mazuri yanafaa kwa masomo.

2.0 KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** na kila Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni siku hiyo bila kukosa akiwa na mahitaji yote ya shule kama ilivyoagizwa.
Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/01/2021**.

3.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni HISABATI,JIOGRAFIA,URAIA,HISTORIA,BIOLOJIA,KEMIA,FIZIKIA,KISWAHILI,KIINGEREZA na somo la Dini ambalo kila Mwanafunzi atahudhuria vipindi vya dini yake.

4.0 VIFAA VYA TAALUMA.

Kila Mwanafunzi atatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:

- Madaftari makubwa kumi.
- Mkebe (Mathematical Set) wenye vifaa vyote ndani yake.
- Kalamu za wino (pen) bluu na nyeusi.
- Penseli na mfuto.
- Rula.
- Dictionary moja.
- Kitabu kimoja cha somo lolote la Sekondari.

5.0 SARE YA SHULE.

5.1 SARE YA WAVULANA.

1. Suruali mbili (02) rangi ya kijani kibichi zilizoshonwa vizuri (**zisizobana**) MODEL (**MODO**)HAZIRUHUSIWI KABISA
2. Shati nyeupe (tetroni) 02 ziwe nza mikono mirefu.
3. Viatu vya ngozi jozi mbili (vya kufunga kwa kamba),(Boots haziruhusiwi kabisa).
4. Soksi jozi mbili (02) rangi nyeusi.
5. Sweta mbili (02) rangi ya kijani kibichi.
6. Tai moja (01) rangi ya kijani.
7. Raba ya michezo na nguo za michezo **(Traksuti ya rangi nyeusi isiyobana/wala kubanwa)**

5.2 SARE YA WASICHANA.

1. Sketi mbili (02) **ndefu zinazokaribia kisigino,** rangi ya kijani kibichi.
2. Blauzi nyeupe mbili (02) za tetroni ziwe na mikono mirefu zisizoonyesha mwili (Transparents)
3. Viatu vya ngozi jozi mbili (02) BOOTS na viatu vyenye visigino virefu (High heels) **HAVIRUHUSIWI KABISA**.
4. Soksi nyeupe jozi mbili (02) au zaidi.
5. Sweta mbili(02) rangi ya kijani kibichi.
6. Tai moja (01) rangi ya kijani.
7. Raba za michezo na nguo za michezo **(Traksuti rangi nyeusi isiyobana/wala kubanwa**).
8. Hijabu rangi nyeupe ivaliwe na suruali rangi ya kijani kibichi kwa Waislamu tu.

6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha,inazingatia Miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafafnuliwa kwa maandishi.

A. Heshima kwa Viongozi,Wazazi,Wanafunzi wote,Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla ni jambo la **LAZIMA**.
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni **LAZIMA.**
C. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.
D. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wanafunzi wapo Shuleni.
E. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na Mazingira ya Shule yaani ndani na nje ya darasa.
F. Kuvaa sare ya Shule wakati wowote uwapo Shuleni.
G. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na
H. Kutunza mali za Umma.

7.0 MAELEZO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA.

A. Inasisitizwa kwamba kila Mwanafunzi aje na mahitaji yote.
B. Kila Mwanafunzi analazimika kutii na kuheshimu Sheria zote na taratibu zake.
C. Kila Mwanafunzi inamlazimu awapo Shuleni kujifunza na kujua wimbo wa Shule,Wimbo wa Taifa, wimbo wa Tanzania nakupenda na Tazama ramani.
D. Kila Mzazi/Mlezi na Mwanafunzi husika inamlazimu kujaza (***KIAMBATISHO B***) kwa ukamilifu na kuleta shuleni mara Shule ifunguapo.
E. Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa (**ni Lazima**).
F. Cheti cha Afya toka kwa Daktari (***KIAMBATANISHO A***).

8.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- Kujichubua na kutumia vipodozi.
- Kukata Sketi ili iwe fupi au kuvaa suruali zinazoonyesha makalio (mlegezo) au suruali zinazobana (model).
- Wizi.
- Uasherati na Ushoga.
- Ubakaji.
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.
- Kupigana au kupiga.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- Kuoa au kuolewa.
- Kutoa mimba.
- Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa Shule au Watu.
- Kukataa adhabu kwa makusudi.
- Kuwa na simu ya mkononi.
  NB: Sheria na taratibu nyingine zote Mwanafunzi atasomewa akifika Shuleni.

09.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHA SHULENI NA MWANAFUNZI.

A. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
B. Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na Sheria,kanuni na maelezo mengine yanayotolewa na Shule.

MWISHO

Unakaribishwa sana **IHONGOLE SEKONDARI** Shule yenye Malengo mazuri Kitaaluma,Kinidhamu na Michezo.

"EDUCATION IS TREASURE"(ELIMU NI HAZINA) Is our MOTTO.

_____

SWENYA H.S

MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO "A"

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI IHONGOLE
S.L.P. 411,
MAFINGA.
18/12/2020.

KUMB.Na.IHSS/MFG/AFYA/F.I/2021.

DAKTARI,
HOSPITALI YA _____
S.L.P. ____
_____

YAH: FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI.

Tafadhali naomba apimwe Mwanafunzi aliyetajwa hapa juu kwa gharama za Mzazi/Mlezi wake na uthibitishe kama anaweza kumudu masomo ya Sekondari katika Shule hii.

Ni muhimu kabla ya kuja hapa ili kujua afya yake.

Nashukuru sana kwa ushirikiano wako.

_____

SWENYA S.H.

MKUU WA SHULE

DAKTARI,
HOSPITALI YA _____,
S.L.P. _____
TAREHE _____

KUMB.NA._____

MKUU WA SHULE,
IHONGOLE SEKONDARI,
S.L.P. 411,
MAFINGA.

YAH: MWANAFUNZI_____

Matokeo ya vipimo vya Mwanafunzi mtajwa hapo juu.

1. Urine_____
2. Stool_____
3. HB_____
4. Spieen_____
5. Chest_____
6. Eyes_____
7. Ears_____
8. Pregnancy Test_____
9. Physical Abnormality_____
10. _____

Nathibitisha kuwa Mwanafunzi huyu

_____
_____
_____

_____	_____	_____	_____
JINA LA DAKTARI	CHEO	SAHIHI	TAREHE

KIAMBATANISHO "B"

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

_____

_____

_____

TAREHE _____

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI IHONGOLE,
S.L.P. 411,
MAFINGA.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHONGOLE

JINA LA MWANAFUNZI _____
KIDATO_____ MWAKA _____

1. Mimi _____Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi hapo juu,nakiri kuwa nimeelewa maelekezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu ajiunge na Shule hii na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kama Mzazi/Mlezi ikiwa ni pamoja na kufuatilia maendeleo yake kwa karibu mara kwa mara na kutii wito pale ninapohitajika shuleni kwa masuala yamhusuyo Mwanangu.
3. Naahidi kumhudumia Mtoto wa kwa hali na mali kwa uwezo wangu wote ili kufanikisha malengo yake ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidi kwamba nitashirikiana vema na Walimu katika kuhakikisha kuwa anafuata sheria na taratibu zote za Shule kama zilivyoainishwa.

JINA LA MZAZI/MLEZI _____SAHIHI_____
ANUANI YA MZAZI/MLEZI_____SIMU_____

Mimi _____
Niliyechaguliwa kujiunga na Shule hii,naahidi kuwa mtiifu kwa Sheria zote za Shule na taratibu zake za kuwa na didhamu ya kujituma kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa Wanafunzi wenzangu ili kufanikisha malengo ya Shule hii.Tofauti na haya niondolewe Shuleni mara moja.

JINA LA MWANAFUNZI_____SAHIHI _____
TAREHE_____